

Nafasi ya Mandhari katika Kukuza Maudhui katika Filamu ya Becky: Uchanganuzi wa Kisemiotiki

Authors

Divinar Nyangarisa ⁽¹⁾; Rose Mavisi ⁽²⁾; Mary Malenya ⁽³⁾

Main author's email: divinarnyangarisa@gmail.com

(1.2) Catholic University of Eastern Africa, Kenya. (3) Kaimosi Friends University College, Kenya.

Cite this article in APA

Nyangarisa, D., Mavisi, R., & Malenya, M. (2026). Nafasi ya mandhari katika kukuza maudhui katika filamu ya Becky: Uchanganuzi wa kisemiotiki. Eastern Africa journal of Kiswahili, 5(1), 181–191. <https://doi.org/10.51317/y62syy48>



A publication of Editon Consortium Publishing (online)

Article history

Received: 2026-07-09

Accepted: 2026-08-12

Published: 2026-09-24

Scan this QR to read the paper online



Copyright: ©2026 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.



Ikisiri

Makala hii ilichanganua namna mandhari inavyofanya kazi kama ishara katika kukuza maudhui katika filamu ya Becky kwa kutumia Nadharia ya Semiotiki. Ingawa tafiti nyingi kuhusu filamu za Kiswahili zimejikita katika lugha, wahusika na ploti, nafasi ya mandhari kama ishara katika kukuza maudhui haijachunguzwa kwa kina katika filamu za Kiswahili nchini Kenya. Utafiti ulitumia muundo wa mchanganyiko wenye mkazo wa ubora, ambapo vipindi 30 kati ya 211 viliteuliwa kwa usampulishaji dhamirifu. Data ilikusanywa kwa kutazama vipindi teule, kunakili mazungumzo yanayohusiana na mandhari na kuchanganua uhusiano kati ya mandhari, vitendo na maudhui. Matokeo yanaonyesha kuwa mandhari ya makazi, kazi, hospitali, polisi, vichakani, makaburini, mandhari ya kidhania na harusi hutumika kama ishara zinazokuza maudhui ya utabaka, kazi, ugonjwa, uhalifu, mauti, tamaa na ndoa. Kwa hiyo, mandhari si usuli wa matukio pekee, bali ni mfumo wa ishara unaoshirikiana na mazungumzo na matendo katika kujenga maana. Makala inapendekeza watayarishaji wa filamu kuzingatia uteuzi na upangaji wa mandhari kama sehemu ya ujenzi wa maudhui, huku tafiti zijazo zikichunguza mwingiliano wa mandhari na mwanga, sauti, muziki, mavazi na upigaji picha. Utafiti huu unaonyesha umuhimu wa mandhari katika kuunganisha fani, maudhui na tajriba ya hadhira katika filamu za mfululizo za Kiswahili.

Maneno muhimu: Filamu, ishara, mandhari, maudhui, semiotiki.

UTANGULIZI

Makala hii ilichanganua namna mandhari inavyofanya kazi kama ishara katika kukuza maudhui katika filamu ya *Becky* kwa kutumia Nadharia ya Semiotiki. Filamu ni mojawapo ya sanaa muhimu za kisasa zinazochanganya fasihi, taswira, sauti na teknolojia katika kuwasilisha ujumbe kuhusu maisha ya binadamu. Ingawa historia yake ilianza na filamu za kimya mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na baadaye ikaingia katika enzi ya sauti na teknolojia za kidijitali, maendeleo haya yameifanya filamu kuwa chombo chenye uwezo mkubwa wa kuunganisha usimulizi na uwasilishaji wa maana kwa njia ya kuona na kusikia (Bordwell & Thompson, 2013; Cook, 2016). Barani Afrika, filamu imeendelea kutoka katika matumizi ya kikoloni hadi kuwa nyenzo ya kujieleza kiutamaduni na kijamii, huku waongozaji kama Ousmane Sembène wakitumia filamu kuibua masuala ya jamii na utambulisho wa Kiafrika (Diawara, 1992; Barlet, 2000).

Nchini Kenya, maendeleo ya tasnia ya filamu yamechangiwa na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia, pamoja na kuenea kwa televisheni za kibinafsi na majukwaa ya kidijitali (Kariuki, 2018). Filamu na tamthilia za televisheni kama *Nairobi Half Life*, *Rafiki*, *Supa Modo*, *Becky*, *Sultana na Zora* zimeonyesha uwezo wa masimulizi ya Kiswahili na masimulizi yanayolenga hadhira ya Kenya kuwasilisha migogoro ya kifamilia, tabaka, mapenzi, tamaa na masuala mengine ya kijamii (Gitonga, 2012; Kahiu, 2018; Wainaina, 2018; Kung'u & Gathigi, 2023). Katika kazi hizi, mandhari si usuli wa matukio pekee. Ni sehemu ya lugha ya kifilamu inayoweza kuonyesha nafasi ya mhusika, kuunda mazingira ya tukio na kuelekeza tafsiri ya ujumbe.

Mandhari hurejelea mazingira ya mahali, wakati na hali ya kijamii yanayozunguka tukio la kisimulizi na kuathiri namna visa vinavyojengeka, wahusika wanavyoendelezwa na maudhui yanavyowasilishwa (Balázs, 1952; Bordwell & Thompson, 2017). Kwa mtazamo wa kisemiotiki, mandhari inaweza kuchanganuliwa kama ishara kwa sababu vipengele vyake vinavyoonekana, kama nyumba, hospitali, barabara, kaburi, seli au eneo la biashara, vinaweza kuhusishwa na dhana na maana zinazozidi matumizi yake ya moja kwa moja. Kwa mfano, nyumba ya kifahari inaweza kuwa kiashiria cha utajiri na hadhi, huku hospitali ikiashiria ugonjwa, ufunuo au utegemezi

kulingana na tukio linalotokea humo. Maana hizo hazitokani na mandhari pekee; hujengwa kupitia uhusiano wake na wahusika, vitendo, mazungumzo na misimbo ya kijamii na kitamaduni (Pramaggiore & Wallis, 2005). Hivyo, mandhari hushiriki katika kugeuza dhana za kimaudhui kuwa uzoefu unaoweza kuonekana na kutafsiriwa na hadhira.

Licha ya umuhimu huo, tafiti nyingi za filamu za Kiswahili nchini Kenya zimejikita zaidi katika lugha, wahusika na maudhui ya jumla, huku nafasi ya mandhari katika ujenzi wa maana ikipewa nafasi ndogo (Wamitila, 2008). Tafiti za Kiafrika zimeonyesha uwezo wa mandhari kuakisi hali za kijamii na kihistoria, lakini sehemu kubwa ya kazi hizo imejikita katika Nollywood, filamu za Tanzania au vipengele vingine vya fani. Nchini Kenya, tafiti za tamthilia za televisheni zimeanza kuchunguza masuala ya kijamii, lakini bado kuna pengo katika uchanganuzi wa kisemiotiki unaolenga moja kwa moja namna mandhari inavyokuza maudhui katika filamu za mfululizo za Kiswahili. Pengo hili ndilo linaloshughulikiwa na makala hii kwa kuchanganua jinsi mandhari katika *Becky* zinavyofanya kazi kama ishara katika ujenzi wa maudhui. Makala inaanza kwa kupitia tafiti zilizotangulia, kisha inaeleza msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti, inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa kuhusisha ushahidi na nadharia, na hatimaye inatoa hitimisho na mapendekezo.

MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti za kimataifa zinaonyesha kwa ujumla kuwa mandhari ni sehemu ya mise-en-scène na inaweza kubeba maana inayochangia ujenzi wa maudhui. Bature-Uzor (2018) alionyesha katika *October 1* kuwa mandhari, mavazi na vifaa vya uigizaji vinaweza kujenga uhalisia wa kihistoria na kuendeleza maudhui ya usaliti wa kikoloni na uovu uliofichwa. Karthick (2023), kwa kutumia mtazamo wa Saussure, alibaini kuwa mandhari ya Pandora katika *Avatar* inaweza kuwasilisha maana za ubeberu wa kiuchumi, tamaa ya rasilimali na ikolojia. Sabol (2018) pia anaonyesha kuwa mandhari ni muundo wa kimawasiliano unaoathiri upokeaji wa maana. Tafiti hizi zinakubaliana kwamba mandhari si mapambo, bali ni sehemu ya usimulizi. Tofauti kuu ni kwamba Bature-Uzor alijikita katika uhalisia wa kihistoria, Karthick katika mandhari ya kubuni na Sabol katika uhusiano wa mandhari na umbo la filamu. Kwa hiyo, bado kuna nafasi ya

kuchunguza namna mandhari za maisha ya kila siku zinavyobeba maana katika filamu za mfululizo za Kiswahili.

Katika tafiti za Kiafrika, Diawara (1992) na Barlet (2000) walionyesha jinsi mandhari ya miji na vijiji ilivyotumiwa kuakisi historia, siasa na hali za kijamii za jamii za Kiafrika. Haynes (2000), katika muktadha wa Nollywood, alihusisha mandhari ya mijini na maudhui kama utajiri wa haraka, uchawi na migogoro ya kifamilia. Tafiti hizi zinakubaliana kwamba mazingira ya filamu yanaweza kuhusishwa na miundo ya kijamii na kiitikadi, lakini hazijajikita katika mfumo mmoja wa kisemiotiki unaochanganua kwa pamoja ishara, maana na nafasi ya hadhira. Aidha, muktadha wa Nollywood na filamu za kihistoria unatofautiana na muktadha wa maisha ya kila siku unaowasilishwa katika *Becky*. Tofauti hii inaonyesha umuhimu wa utafiti unaochanganua mandhari katika mfululizo wa Kiswahili wa Kenya kwa kuzingatia mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika.

Katika Afrika Mashariki, Kariuki na Kamwara (2025) walibaini kuwa mandhari halisi na ya kufikirika katika *Tumaini* na *Kala Tufaha* hushirikiana katika ujenzi wa maudhui, lakini utafiti wao ulijikita katika riwaya andishi. Ntongai na wenzake (2025) walichunguza aina za mandhari katika Nguu za Jadi kwa mkabala wa kifinominojia, wakisisitiza tajriba ya ndani ya wahusika. Tafiti hizi zinaonyesha kuwa mandhari ni kipengele muhimu cha uchanganuzi wa fasihi ya Kiswahili, lakini zinatofautiana na utafiti huu kwa aina ya matini na mkabala wa kinadharia. Tofauti hiyo ni muhimu kwa sababu filamu huunganisha mandhari na taswira, sauti, mwendo na mazungumzo, hivyo maana ya mandhari inaweza kujengwa kwa njia tofauti na katika riwaya.

Nchini Kenya, Kung'u na Gathigi (2023) walionyesha kuwa tamthilia za televisheni zenye wahusika wa kike huibua masuala kama umaskini, ufiadini, ndoa, wivu na migogoro ya kifamilia. Hata hivyo, utafiti wao haukulenga mandhari wala kutumia uchanganuzi wa kisemiotiki. Karata na wenzake (2021) nao walionyesha kuwa mkabala wa kiishara unaweza kutumika kufasiri vitu na matukio katika fasihi ya Kiswahili, ingawa hawakulenga filamu au mandhari moja kwa moja. Kwa jumla, tafiti hizi zinaonyesha maeneo mawili yanayokutana: umuhimu wa mandhari katika ujenzi wa maudhui na uhalali wa mkabala wa kiishara katika

fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, bado kuna pengo la tafiti zinazounganisha maeneo hayo mawili katika uchanganuzi wa filamu ya mfululizo ya Kiswahili nchini Kenya.

Kwa msingi huo, makala hii inashughulikia pengo hilo kwa kuchanganua *Becky* kwa kutumia mfumo unaounganisha dhana za Saussure, Peirce na Barthes. Tofauti na tafiti zilizotangulia, uchanganuzi huu unaangalia mandhari kama ishara inayojengwa katika mwingiliano wa mazingira, vitendo, mazungumzo, misimbo ya kijamii na tafsiri ya hadhira. Mtazamo huo unawezesha kubainisha si tu aina za mandhari zinazojitokeza katika *Becky*, bali pia namna zinavyokuza maudhui katika muktadha wa kijamii na kiuchumi wa Kenya.

Kwa jumla, mapitio haya yanaonyesha kuwa tafiti zilizotangulia zimeweka msingi wa kuelewa mandhari kama kipengele cha ujenzi wa maana, lakini hazijaunganisha kwa kina uchanganuzi wa mandhari, semiotiki na filamu za mfululizo za Kiswahili nchini Kenya. Hivyo, utafiti huu unalenga kuchanganua namna mandhari katika *Becky* zinavyofanya kazi kama ishara katika kukuza maudhui.

Msingi wa Nadharia

Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Semiotiki, inayohusu jinsi ishara zinavyounda na kuwasilisha maana katika mifumo mbalimbali ya mawasiliano. Katika utafiti huu, dhana za Ferdinand de Saussure, Charles Sanders Peirce na Roland Barthes hazitumiki kama nadharia zinazojitegemea, bali kama mihimili inayokamilishana ndani ya mfumo mmoja wa uchanganuzi. Saussure anatoa msingi wa kutambua ishara na uhusiano kati ya kiashiria na kinachoashiriwa; Peirce anaongeza mchakato wa uashiraji unaohusisha ishara, kirejelea na mfasiri; na Barthes anaeleza namna misimbo ya kijamii na kitamaduni inavyopanua maana ya ishara. Muunganiko huu unawezesha utafiti kuanzia katika kutambua mandhari inayoonekana, kueleza maana inayohusishwa nayo, kuchunguza muktadha unaoipa maana hiyo uhalali na hatimaye kueleza namna hadhira inavyoweza kuitafsiri.

Semiotiki inafaa katika uchanganuzi wa mandhari kwa sababu mandhari ya kifilamu huwasilishwa kwa njia ya taswira na huwekwa katika uhusiano na wahusika, vitendo, mazungumzo, sauti na mazingira mengine. Kwa hiyo, mandhari inaweza kuwa ishara pale

kipengele chake kinachoonekana kinapobeba dhana au ujumbe unaozidi maana yake ya moja kwa moja. Kwa mfano, nyumba ya kifahari inaweza kuwa kiashiria cha makazi, lakini ndani ya muktadha wa *Becky* inaweza pia kuashiria utajiri, mamlaka au utabaka. Maana hiyo haipatikani katika nyumba yenyewe pekee; hujengwa na namna inayohusishwa na wahusika na matukio. Hivyo, uchanganuzi wa mandhari katika makala hii unazingatia kwa pamoja umbo linaloonekana, maana inayohusishwa nalo, msimbo wa kijamii unaoliongoza na mchakato wa tafsiri.

Kwa madhumuni ya uchanganuzi, mfumo huu umetafsiriwa katika mihimili minne inayohusiana: (1) ishara, (2) kiashiria na kinachoashiriwa, (3) misimbo ya kijamii na kitamaduni, na (4) mfumo wa pande tatu wa Peirce. Mihimili hiyo haichanganui vipengele vinavyotengwa, bali hatua zinazofuatana katika kujenga maana. Kwanza, mtafiti alitambua mandhari kama ishara; pili, alifafanua kile kinachoonekana na dhana inayowakilishwa; tatu, alichunguza misimbo inayofanya uhusiano huo kueleweka katika muktadha wa jamii; na nne, hueleza namna mfasiri au hadhira anavyoweza kujenga maana kutokana na ishara hiyo.

Ishara: Kwa mujibu wa Saussure (2011), ishara huundwa na muungano wa umbo linaloonekana na maana inayohusishwa nalo. Katika *Becky*, nyumba za kifahari, mitaa ya mabanda, hospitali na seli za polisi zinaweza kutambuliwa kama ishara kwa sababu zinahusishwa na dhana kama utajiri, hali ya chini ya kiuchumi, ugonjwa, udhibiti au adhabu. Mhimili huu hutumika kutambua kipengele cha mandhari kinachobeba maana kabla ya kuchanganua uhusiano wake na maudhui.

Kiashiria na kinachoashiriwa: Saussure (2011) anatofautisha kiashiria, yaani umbo linalowasilishwa, na kinachoashiriwa, yaani dhana inayowakilishwa. Kwa mfano, nyumba ya kifahari ni kiashiria, ilhali hadhi ya kijamii na kiuchumi inayohusishwa nayo ni kinachoashiriwa. Uhusiano huu si wa asili bali hujengwa katika muktadha wa kijamii na kitamaduni. Mhimili huu husaidia kueleza kwa nini mandhari moja inaweza kupata maana tofauti kulingana na tukio, mhusika na muktadha.

Mfumo wa msimbo: Barthes (1972, 1977) anaonyesha kuwa maana ya ishara za kisanaa hujengwa pia kupitia

misimbo ya kijamii na kitamaduni inayotambulika na hadhira. Katika *Becky*, mwanga hafifu, giza, ukimya na mpangilio wa nafasi vinaweza kuimarisha tafsiri ya hatari, huzuni, adhabu au msiba. Mhimili huu unaonyesha kwamba maana ya mandhari haijengwi na taswira pekee, bali pia na matarajio na maarifa ya kitamaduni yanayomsaidia mtazamaji kuitafsiri.

Uundaji wa maana kupitia mfumo wa pande tatu wa Peirce: Peirce (1931–1958) anaongeza mwelekeo wa mfasiri katika mchakato wa uashiraji. Katika mfumo huu, ishara hujenga uhusiano na kirejelea na kuzalisha tafsiri kwa mfasiri. Kwa mfano, mandhari ya kaburi inaweza kurejelea kifo, lakini maana inayotokana nayo inaweza kuwa majonzi, kumbukumbu, udanganyifu au kutafuta mwongozo kulingana na tukio na mazungumzo yanayohusiana nayo. Mhimili huu unawezesha utafiti kueleza kwa nini ishara hiyo inaweza kuzalisha maana tofauti katika matukio tofauti.

Kwa hiyo, mihimili hii inatumika kwa mtiririko unaokamilishana. Uchanganuzi ulianza kwa kutambua mandhari kama ishara, kisha ulionyesha uhusiano kati ya kiashiria na kinachoashiriwa, ulichunguza misimbo ya kijamii na kitamaduni inayopanua maana, na hatimaye ulieleza nafasi ya mfasiri katika kuijenga maana hiyo. Mfumo huu ndio uliotumika katika uchanganuzi wa matokeo, hivyo unaleta uhusiano wa kimantiki kati ya Saussure, Peirce na Barthes badala ya kuwachukulia kama mifumo isiyohusiana. Mfumo huu ndio unaotumika katika uchanganuzi wa matokeo, hivyo unaleta uhusiano wa kimantiki kati ya Saussure, Peirce na Barthes badala ya kuwachukulia kama mifumo isiyohusiana.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa mchanganyiko wenye mkazo wa ubora, ukichanganya uwasilishaji wa kimaielezo wa data na uchanganuzi wa kifasihi na kisemiotiki wa filamu. Kipengele cha kimaielezo kilitumika kuonyesha idadi na mgawanyo wa vipindi vilivyoteuliwa, huku uchanganuzi wa ubora ukieleza maana ya mandhari, mazungumzo na matendo katika matukio husika. Eneo la utafiti lilikuwa filamu zinazozalishwa nchini Kenya, huku *Becky* ikiteuliwa kama kielelezo kwa sababu ina matukio mengi yanayohusisha mandhari na maudhui ya kijamii na kiuchumi yanayohusiana na maisha ya wahusika wa

mijini. Filamu iliteuliwa kwa usampulishaji dhamirifu (Creswell, 2014; Mugenda & Mugenda, 1999).

Kutoka jumla ya vipindi 211, vipindi 30 viliteuliwa kwa usampulishaji dhamirifu kwa kuzingatia vigezo vinne. Kwanza, mandhari ilipaswa kutambulika wazi katika tukio; kwa mfano, nyumba, hospitali, kituo cha polisi au eneo la biashara. Pili, mandhari ilipaswa kuhusishwa na kitendo, mazungumzo au mabadiliko muhimu ya simulizi. Tatu, tukio lilipaswa kutoa ushahidi wa moja kwa moja wa maudhui yaliyolengwa, kama utabaka, kazi, ugonjwa au uhalifu. Nne, tukio lilipaswa kuwa na data ya kutosha ya kifilamu inayoweza uchanganyuzi wa kisemiotiki. Data ilikusanywa kwa kutazama vipindi teule kwa makini, kurejelea matukio mara kwa mara na kunakili mazungumzo yanayohusiana na mandhari. Kwa hatua hizi, vigezo vya uteuzi vilitumika kwa namna inayoweza kufuatiliwa katika kila kipindi kilichojumuishwa.

Kuhusu maadili na matumizi ya kazi yenye hakimiliki, uchambuzi ulifanywa kwa madhumuni ya kitaaluma na kwa kuzingatia uadilifu wa utafiti. Dondoo za mazungumzo zilitumika kwa kiwango kinachohitajika kueleza hoja za uchanganyuzi, na vipindi vilitambuliwa kwa nambari ili kurahisisha ufuatiliaji wa ushahidi. Utafiti haukusudiwa kusambaza tena filamu nzima wala kuiga kazi yake kwa matumizi ya kibiashara. Waandishi waliheshimu haki za waandishi, waigizaji, waongozaji na wamiliki wa kazi kwa kutambua chanzo cha matini iliyochanganuliwa na kuepuka matumizi yasiyohitajika ya maudhui. Kwa kuwa utafiti haukuhusisha washiriki wa kibinadamu, masuala ya ridhaa ya washiriki hayakuhusika moja kwa moja.

MATOKEO YA UTAFITI

Maudhui ni kiini cha kazi ya sanaa; ni ujumbe, wazo kuu au somo linaloipa kazi husika mwelekeo na maana (Senkoro, 1982). Sehemu hii inawasilisha matokeo ya uchanganyuzi wa makundi saba ya kimaudhui na aina nane za mandhari zilizobainika katika vipindi 30 vya *Becky*. Ushahidi wa msingi unatokana na matukio, mandhari na dondoo za mazungumzo, huku tafsiri ya kisemiotiki ikiwasilishwa kwa kuzingatia mihimili iliyofafanuliwa katika sehemu ya Msingi wa Nadharia.

Mandhari na Maudhui ya Utabaka

Utabaka, kwa mujibu wa Wamitila (2003), hujitokeza pale mtunzi anapoonyesha tofauti za kimaisha baina

ya wahusika zinazoweza kusababisha migongano, dharau au chuki. Katika *Becky*, utabaka hujengwa kupitia mandhari ya makazi na nafasi ambazo wahusika wanaruhusiwa kuchukua. Katika kipindi cha kwanza, *Becky* anaonekana akifanya kazi ya usafi katika jumba la Martha Katana, mazingira yanayotofautiana na maisha yake katika eneo la kipato cha chini. Jumba lenye ukubwa, mapambo na vifaa vya kifahari ni kiashiria, ilhali utajiri na mamlaka vinavyohusishwa nalo ni kinachoashiriwa. Kwa upande mwingine, makazi ya *Becky* yanaashiria hali ya chini ya kiuchumi. Huu ni mfano wa kisemiotiki unaoonyesha jinsi mandhari inavyogeza tofauti ya mali kuwa maana ya kijamii ya utabaka.

Ushahidi wa filamu unaonyesha kuwa utabaka katika *Becky* haujengwi kwa tofauti ya mali pekee, bali pia kwa mipaka ya kijamii. Katika kipindi cha 4, Trisha anapomuona Junior akimtaazama *Becky* kutoka ghorofani, anamwambia: "... mimi na wewe hatufai kuwa concerned na such people" (Kip. 4). Kauli hii inatolewa katika mazingira ya jumba la familia ya Martha na inaunganisha nafasi ya kimwili na nafasi ya kijamii. *Becky* yupo ndani ya jumba hilo kwa sababu ya kazi, lakini kauli ya Trisha inaonyesha kuwa uwepo wake haumfanyi ahesabiwe kuwa sehemu ya familia. Hivyo, mandhari inafanya mpaka wa kitabaka uonekane hata pale wahusika wanaposhiriki nafasi moja.

Uhusiano huu unaonekana pia katika tukio la *Becky* kugundua dawa katika chumba cha Martha. Katika kipindi cha 10, *Becky* anapokuwa akifanya usafi katika chumba cha Martha, anakutana na dawa za mwajiri wake. Martha anapoingia na kumwona *Becky* karibu na vitu vyake binafsi, anamfukuza akisema: "What did I tell you about snooping around! You are fired! Nisijirudie tena, Leave!!" (Kip. 10). Chumba cha binafsi kinakuwa kiashiria cha mpaka kati ya mwenye mali na mfanyakazi. Tukio hili linaonyesha kuwa kuwa ndani ya jumba hakumaanishi kuwa wahusika wana mamlaka sawa juu ya nafasi hiyo.

Mandhari na Maudhui ya Kazi

Kazi, kama maudhui ya kifasihi, hurejelea shughuli anazozifanya mhusika ili kujikimu kimaisha au kutimiza wajibu wake katika jamii, na mara nyingi huakisi hali ya ajira na mahusiano ya kikazi (Senkoro, 1982). Katika *Becky*, mandhari ya sehemu za kazi hutumika kama

ishara ya nafasi ya mhusika katika jamii, hali yake ya kiuchumi na mahusiano ya kimamlaka. Katika kipindi cha kwanza, *Becky* anaanza kazi ya ujakazi katika jumba la Martha. Katika kipindi cha pili, *Sally* na Martha wanakagua kazi yake na *Sally* anasema, “Good job!”, naye *Becky* anauliza, “For real?” (Kip. 2). Tukio hili linaonyesha mahali pa kazi kama nafasi ya kuthibitisha uwezo na kujenga njia ya kujitegemea. Katika kipindi cha 171, Hakim anamkaribisha *Becky* amfanyie usafi nyumbani kwake, akisema: “Twende Kwangu ukanifanyie usafi, manake yule dada anayenifanyia hajakuja...” (Kip. 171). Ushahidi huu unaonyesha kazi kama njia ya *Becky* ya kujipatia riziki.

Mandhari ya kazi pia inaonyesha uhusiano kati ya ajira, hadhi na fursa. Katika jumba la Martha, mazingira ya kifahari yanaonyesha tofauti kati ya mwenye mali na mfanyakazi anayehudumia mali hiyo. Katika kampuni ya Hakim, inayotajwa katika kipindi cha 173, mazingira ya kazi yanaashiria ajira rasmi na uwezekano wa kubadilika kwa hali ya kiuchumi. Hakim anamweleza *Becky*: “Well I have this clearing and forwarding company and the person that was employed to do this job has decided to take it for granted and it’s very frustrating...” (Kip. 173). Kwa hiyo, mandhari ya kazi haionyeshi shughuli ya ajira pekee, bali pia nafasi, mamlaka na uwezekano wa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Ushahidi wa Tito unaimarisha hoja hii. Katika kipindi cha 6, filamu inaonyesha kibanda chake kidogo cha kuuza supu na mutura, huku bango lenye maandishi “TITO’S MUTURA BASE” likitambulisha biashara hiyo. Mazingira hayo yanaambatana na mazungumzo yake na wateja, yakiwemo mazungumzo na Shantel katika kipindi cha 7, ambapo Shantel anasema: “Si unifungie ya soo nianze nayo...” (Kip. 7). Kibanda, bango na shughuli ya kuuza chakula vinafanya kazi kama viashiria vya uchumi wa kujikimu. Mandhari haya yanaonyesha kazi ya kila siku kama mkakati wa kujipatia riziki katika mazingira yenye fursa ndogo za kiuchumi.

Mandhari ya kazi pia yanaibua matumizi ya mamlaka na utegemezi. Katika simulizi inayohusu kazi ya *Sally* hospitalini, mazingira ya kazi yanaonyesha kuwa ajira inaweza kuathiriwa na watu wenye ushawishi. Aidha, katika vipindi vya 103 na 106, mabadiliko ya nafasi ya Junior katika kampuni na makazi yake yanaonyesha

jinsi kupoteza mali kunavyoweza kusababisha kupotea kwa hadhi na fursa za kiuchumi. Kwa hiyo, mandhari ya kazi yanaonyesha kuwa ajira si chanzo cha kipato pekee; ni pia eneo ambalo mamlaka, tabaka na fursa hukutana.

Mandhari na Maudhui ya Ugonjwa

Ugonjwa, kama maudhui ya kifasihi, hutumika kuwasilisha udhaifu wa kibinadamu, hali za kihisia na mabadiliko ya kimaisha. Katika *Becky*, mandhari ya hospitali inafanya kazi kama ishara ya matibabu, ufunuo na mabadiliko ya taarifa. Katika kipindi cha 14, Tito anapoteza fahamu akiwa kazini na baadaye anajikuta hospitalini. Sanchez anamweleza: “Uko hosi bro”, na Tito anauliza, “Hosi aje tena?”, kabla Sanchez kueleza kuwa “ulicollapse pale biz...” (Kip. 14). Katika kipindi cha 19, Martha anaenda hospitalini baada ya kuanguka na daktari anamweleza: “I have done a CT scan, MRI test and there’s nothing; no tumour, no cancer” (Kip. 19). Katika matukio haya, hospitali si mahali pa matibabu pekee; ni mazingira ambamo taarifa kuhusu afya zinabadilika na siri zinaweza kufichuka.

Mandhari ya hospitali pia huunganisha ugonjwa na mahusiano ya kijamii. Katika kipindi cha 14, hospitali inawaunganisha Tito, Sanchez na Sally, huku Sally akipata taarifa muhimu kuhusu ajali iliyomhusisha Tito. Katika kipindi cha 55, Trisha anaishia hospitalini baada ya kujifanya amepoteza mtoto ambaye hajazaliwa, na daktari anamshauri Martha kuhusu mapumziko na mazingira yanayoweza kuathiri hali yake. Hivyo, hospitali inakuwa kiashiria kinachounganisha afya, mahusiano, udanganyifu na maslahi binafsi.

Katika tukio la Martha, hospitali inabadilisha uelewa wa hadhira kuhusu hali yake. Baada ya CT scan na MRI, daktari anathibitisha kuwa “there’s nothing; no tumour, no cancer” (Kip. 19). Kwa mtazamo wa Peirce, maana ya hospitali hapa hujengwa na uhusiano kati ya ishara ya mazingira, tukio la vipimo na tafsiri ya hadhira. Kwa hiyo, mandhari ya hospitali inakuwa sehemu ya mchakato wa kufichua ukweli na kusogeza mbele fumbo la simulizi.

Ugonjwa wa Jeff unaongeza mwelekeo wa kiuchumi na kifamilia. Katika kipindi cha 10, *Becky* na *Moreen* wanazungumza kuhusu hali ya Jeff na gharama za dawa na sindano. *Moreen* anasema kuwa ameweza

kupata “500 bob” ya kununua dawa, lakini bado inahitajika fedha zaidi kwa sindano zilizobaki (Kip. 10). Mandhari yanayohusiana na matibabu yanaunganisha ugonjwa na uwezo wa kifedha wa familia. Hivyo, ugonjwa unaonyeshwa si kama hali ya mwili pekee, bali kama mzigo unaoathiri mahusiano, fedha na wajibu wa wahusika.

Mandhari na Maudhui ya Uhalifu

Uhalifu ni maudhui yanayojitokeza pale wahusika wanapovunja sheria au kanuni za kijamii, hali inayoweza kusababisha adhabu na mfarakano (Wamitila, 2003). Katika *Becky*, seli za polisi na maeneo ya vichakani hutumika kama ishara za kupoteza uhuru, udhibiti na hatari. Katika kipindi cha 197, Trisha anakamatwa na kupelekwa katika mazingira ya polisi. Anasema: “You guys have no idea who you are dealing with. I need to make a phone call”, huku askari akimkumbusha kuwa ana haki ya kupiga simu moja (Kip. 197). Mandhari ya seli ni kiashiria cha kupoteza uhuru na kuingia chini ya udhibiti wa sheria. Katika kipindi cha 208, Pupa pia anakamatwa na askari anamwambia: “Uko under arrest. Kwa kuvunja nyumba za watu na kuiba unreasonable amount of money. Kwanza kuna mtu alikufa...” (Kip. 208).

Mandhari ya seli na vichakani yanatofautiana na mandhari ya nyumbani kwa sababu yanawakilisha kuvurugika kwa maisha ya kawaida. Katika kipindi cha 200, *Becky* anatekwa nyara na kupelekwa vichakani. Mazingira hayo yanamtoa katika nafasi yake ya kawaida na kumweka katika hali ya hatari na kutengwa. Kwa mtazamo wa Barthes, seli na mazingira ya polisi yanaweza kusomwa kama misimbo ya udhibiti na adhabu, huku vichakani vikijenga msimbo wa hatari na kutokuwa na usalama.

Ushahidi wa Trisha unaonyesha kuwa mandhari hubadilisha maana ya mamlaka. Akiwa katika kituo cha polisi, anasema: “You guys have no idea who you are dealing with. I need to make a phone call” (Kip. 197). Kauli hii inaonyesha jaribio la kutumia hadhi na mtandao wake wa kijamii hata katika mazingira ya kizuizi. Hata hivyo, askari anamwelekeza kufuata utaratibu wa kituo. Hivyo, mandhari ya polisi inaweka wazi mgongano kati ya mamlaka binafsi na mamlaka rasmi.

Katika utekaji wa *Becky*, vichakani vinakuwa ishara ya hatari na kutengwa. Katika kipindi cha 200, *Becky* anasikika akisema: “Niacheeee! Niacheeee!”, huku mtekaji akimwamuru: “Nyamanza! Nyamanza!” (Kip. 200). Mazingira ya vichakani, pamoja na mazungumzo hayo, yanajenga hali ya hofu na kutokuwa na usalama. Kwa hiyo, mandhari ya uhalifu huimarisha hisia za tukio na kuonyesha matokeo ya migogoro iliyojengwa katika mandhari za awali.

Mandhari na Maudhui ya Mauti

Mauti ni mojawapo ya maudhui yanayojitokeza katika kazi za fasihi na sanaa, yakihusishwa na majonzi, kumbukumbu, msamaha na maamuzi ya kimaisha. Katika *Becky*, mandhari ya makaburi huonyesha maana tofauti za mauti kulingana na muktadha. Katika kipindi cha 44, Trisha anamwomba Vicky amtafutie kaburi la kughushi na kusema: “Nataka uende kwa graveyard unitafutie grave yoyote yenye tarehe ya leo...” (Kip. 44). Hapa kaburi linakuwa kiashiria cha udanganyifu. Kinyume chake, katika kipindi cha 198, *Becky* anatembelea kaburi la mama yake na kusema: “...kuna Junior mwenye amesacrifice everything to prove our love... na mimi mum nimempromise it is us against the world, so naneed guidance...” (Kip. 198). Hapa kaburi linakuwa ishara ya kumbukumbu na kutafuta mwongozo.

Mandhari ya makaburi kwa hiyo inatofautisha mauti ya kweli na mauti ya kubuniwa. Katika kipindi cha 44, kaburi linatumika kuficha uongo kuhusu kifo cha mama wa Trisha; katika kipindi cha 198, linakuwa mahali pa *Becky* kutafuta mwongozo. Ishara hiyo hiyo hupata maana tofauti kutokana na muktadha wa mhusika, kitendo na mazungumzo. Hii inaonyesha umuhimu wa kuchanganua mandhari pamoja na vipengele vingine vya tukio badala ya kuipa maana moja isiyobadilika.

Katika ziara ya *Becky*, mazungumzo yake na mama yake aliyefariki yanaunganisha kumbukumbu na maamuzi ya sasa. Katika kipindi cha 198, *Becky* anasema kuwa Junior “amesacrifice everything to prove our love” na kwamba yeye “naneed guidance” (Kip. 198). Kwa mtazamo wa Peirce, kaburi linakuwa ishara inayozalisha maana kupitia muktadha wa mazungumzo na kumbukumbu. Hivyo, mauti yanaendelea kuwa na athari katika maisha ya wahusika hata baada ya tukio la kifo.

Kwa Lexy, kaburi la baba yake linafungua historia ya familia na majuto ya kutokujua ukweli mapema. Katika kipindi cha 211, Lexy anasema: “Sahihi tu ingekuwa ni tears of joy, si ya pain na regrets. I wish ungelive long tucreate more memories...” (Kip. 211). Kauli hii inaonyesha namna mandhari ya kaburi yanavyobeba hisia za wakati uliopotea. Hivyo, mandhari ya mauti yanaunganisha wakati uliopita na wa sasa na kuendeleza maudhui ya familia, majuto, kumbukumbu na msamaha.

Mandhari na Maudhui ya Tamaa

Tamaa ni hamu kubwa ya kutaka kupata kitu, mara nyingi mali, madaraka au mapenzi, hata kwa njia zisizo halali (Wamitila, 2003). Katika *Becky*, tamaa hujengwa kupitia mandhari ya kidhania na tofauti za kimazingira. Katika kipindi cha 46, Trisha akiwa jikoni akinyemelea mkoba wa *Becky* na kuchukua mkufu wake, anajisemea: “I don't care what happened, but there is no way I will allow such a loser to own what is rightfully mine” (Kip. 46). Kauli hii inaonyesha kuwa tamaa imeanza katika fikra kabla ya kudhihirika kwa kitendo. Mandhari ya ndani, pamoja na kujisemeza kwa Trisha, inakuwa ishara ya nia iliyofichika na kumwezesha mtazamaji kufahamu motisha ya mhusika.

Tamaa pia inajengwa kupitia tofauti kati ya mazingira ya maisha. Katika kipindi cha 105, Moreen anakataa kurudi katika maisha ya ghetto na kusema: “ghetto for me is a big no!” (Kip. 105). Katika kipindi cha 119, anasisitiza: “mimi sitaacha lifestyle yangu fiti kurudi hapa niteseke sawa, never ever!” (Kip. 119). Kauli hizi zinaonyesha kuwa baada ya kuzoea mazingira ya kifahari, ghetto inakuwa kiashiria cha hali anayotaka kuikimbia, huku maisha ya juu yakiwa kiashiria cha hadhi anayotaka kuendelea kuimiliki.

Tamaa inapofikia hatua ya kuhusishwa na madhara kwa wengine, mandhari ya kifahari hupata maana mpya. Katika kipindi cha 190, Sanchez anasema: “sikuwahi dhani hadi unaweza mada msee juu ya greed na mali...” (Kip. 190), akifichua uhusiano kati ya tamaa na matendo hatari. Kwa mtazamo wa semiotiki, nyumba na mali ni viashiria vinavyounganisha utajiri na matarajio ya wahusika. Mnyororo wa maana unaonekana kutoka katika kuona maisha ya juu, kuyatamani na hatimaye kuchukua hatua zisizofaa kuyapata.

Mandhari na Maudhui ya Ndoa

Ndoa ni taasisi ya kijamii inayounganisha watu wawili kisheria na kimaadili, ikiwa na majukumu na matarajio mahususi kwa kila mwenza (Wamitila, 2003). Katika *Becky*, mandhari ya maandalizi ya harusi na maisha ya nyumbani hutumika kuibua maudhui ya ndoa. Katika kipindi cha 11, Trisha na Junior wanaonekana katika duka la Devine Collections wakifanya maandalizi ya harusi. Nguo za harusi, vioo na viatu vilivyopangwa vinaashiria maandalizi ya muungano unaotarajiwa kutambuliwa na jamii. Hata hivyo, mandhari hayo yanaambatana na migogoro ya ndani kwa sababu hisia za Junior kwa *Becky* bado zipo. Katika kipindi cha 56, Trisha anaonyeshwa akishindwa kufanya baadhi ya kazi za nyumbani kama kupika na kuosha nguo za Junior. Tofauti hii inaonyesha pengo kati ya matarajio ya kijamii kuhusu ndoa na hali halisi ya mahusiano.

Katika kipindi cha 11, msimamizi wa duka anamwambia Shantel: “...msaidie Trisha kufanya Shopping” (Kip. 11), huku mazingira ya duka yakionyesha bidhaa za maandalizi ya harusi. Mandhari haya yanaashiria ndoa kama taasisi inayotayarishwa na kutambulishwa hadharani. Kwa upande mwingine, mazingira ya nyumbani katika kipindi cha 56 yanaonyesha changamoto za majukumu na mahusiano. Kwa hiyo, mandhari ya ndoa hayajengi taswira ya sherehe pekee, bali yanafunua pia matarajio, migogoro na majukumu yanayohusishwa na maisha ya ndoa.

Majadiliano

Matokeo yanaonyesha kuwa mandhari katika *Becky* hufanya kazi kama sehemu ya ujenzi wa maana badala ya kuwa usuli wa matukio. Katika makundi yote saba ya kimaudhui, mazingira yanaweka wahusika katika nafasi maalumu za kijamii na kiuchumi, huandaa migogoro na huathiri namna hadhira inavyotafsiri matukio. Kwa mfano, jumba la Martha na makazi ya *Becky* yanafanya tofauti ya mali ioneke kama tofauti ya hadhi na mamlaka. Vilevile, hospitali, seli, vichakani na makaburini hupeua maana zinazobadilika kulingana na kitendo na mazungumzo yanayotokea humo.

Hoja hii inaendana na Pramaggiore na Wallis (2005), wanaonyesha kuwa mandhari ni sehemu ya muundo wa filamu inayosaidia hadhira kuelewa maana ya simulizi. Pia inaafikiana na Bature-Uzor (2018), ambaye alibaini kuwa vipengele vya mazingira vinaweza kubeba maana ya kihistoria na kisanaa. Hata hivyo,

utafiti huu unaongeza mwelekeo mwingine kwa kuonyesha kuwa hata mandhari ya kawaida ya maisha ya kila siku, kama ghetto, kibanda cha biashara, nyumba na hospitali, zinaweza kufanya kazi kama ishara zenye uzito wa kimaudhui. Tofauti hii inahusiana na muktadha wa Becky kama filamu ya mfululizo inayosimulia maisha ya kawaida ya wahusika katika mazingira ya mijini.

Kwa mtazamo wa Saussure, matokeo yanaonyesha uhusiano kati ya kiashiria na kinachoashiriwa. Nyumba ya kifahari inaweza kuwa kiashiria cha mazingira ya kuishi, lakini katika muktadha wa matukio husika huashiria pia utajiri, mamlaka na utabaka. Kwa mtazamo wa Barthes, misimbo ya kijamii na kitamaduni huongeza maana hiyo kupitia mpangilio wa nafasi, mwanga, giza na mazingira ya tukio. Kwa upande wa Peirce, maana haikamiliki katika mandhari yenyewe, bali hujengwa kupitia uhusiano wake na tukio, kirejelea na mfasiri. Kwa hiyo, kaburi linaweza kuashiria udanganyifu katika tukio moja na kumbukumbu au mwongozo katika tukio jingine. Muunganiko wa mihimili hii unaonyesha kwa nini maana ya mandhari haiwezi kutenganishwa na muktadha.

Matokeo pia yanaonyesha mchango wa utafiti katika kupanua uchanganuzi wa filamu za Kiswahili kutoka katika kusimulia ploti na kutambua maudhui hadi kuchunguza namna fani inavyobeba maana. Mandhari katika Becky huunganisha fani na maudhui kwa kufanya dhana kama utabaka, ugonjwa, uhalifu, mauti na tamaa zionekane katika mazingira maalumu. Hivyo, mabadiliko ya mandhari yanaweza pia kuashiria mabadiliko ya mahusiano na hadhi za wahusika. Kwa mfano, Junior anapohama kutoka jumba la familia hadi ghetto, mabadiliko ya mazingira yanaambatana na mabadiliko ya hali yake ya kiuchumi na kijamii; vivyo hivyo, Trisha anapohama kutoka mazingira ya starehe hadi selini, nafasi yake ya kijamii na mamlaka hubadilika.

Kwa ujumla, matokeo yanaonyesha kuwa mandhari hufanya kazi kwa kushirikiana na mazungumzo na matendo, lakini haipotezi hadhi yake kama kipengele huru cha fani. Maana hujitokeza kutokana na mwingiliano wa mazingira na vipengele vingine vya kifilamu. Kwa hiyo, uchanganuzi wa mandhari unapaswa kuangalia si eneo pekee, bali pia mfuatano

wa mazingira, muktadha wa tukio na namna hadhira inavyopewa nafasi ya kutafsiri ishara. Mtazamo huu unaimarisha hoja kwamba mandhari ni sehemu hai ya usimulizi na inaweza kuwa kiungo kati ya fani, maudhui na tajriba ya hadhira.

Mapungufu ya Utafiti

Utafiti huu una mapungufu mawili makuu. Kwanza, ulihusisha filamu moja tu, Becky, na vipindi 30 vilivyoteuliwa kutoka katika vipindi 211; kwa hiyo, matokeo haya yanapaswa kueleweka ndani ya muktadha wa kazi hiyo na hayawezi kuwakilisha filamu zote za Kiswahili nchini Kenya. Pili, uchanganuzi ulijikita zaidi katika mandhari na uhusiano wake na maudhui, hivyo haukuchanganua kwa kina mwingiliano wa mandhari na vipengele vingine vya kifilamu kama mwanga, sauti, muziki, mavazi na upigaji picha. Mapungufu haya yanaonyesha maeneo ambayo tafiti zijazo zinaweza kuyapanua.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala hii imechanganua namna mandhari inavyofanya kazi kama ishara katika kukuza maudhui katika filamu ya Becky kwa kutumia Nadharia ya Semiotiki. Uchambuzi wa vipindi 30 kati ya 211 umeonyesha kuwa makundi saba ya kimaudhui yaliengwa kupitia aina mbalimbali za mandhari, zikiwemo makazi, maeneo ya kazi, hospitali, kituo cha polisi, vichakani, makaburini, mandhari ya kidhania na harusi. Mandhari hizo hushiriki katika kujenga maudhui ya utabaka, kazi, ugonjwa, uhalifu, mauti, tamaa na ndoa.

Kwa msingi huo, tafiti zijazo zinapendekezwa kuchunguza mwingiliano wa mandhari na mwanga, sauti, muziki, mavazi na upigaji picha katika filamu za mfululizo za Kiswahili. Uchunguzi mpana zaidi wa filamu nyingi na vipindi zaidi unaweza pia kusaidia kulinganisha namna mandhari zinavyobeba maana katika muktadha tofauti ya kijamii na kiutamaduni.

Mapendekezo: Kutokana na matokeo ya utafiti huu, watayarishaji na waongozaji wa filamu za mfululizo za Kiswahili nchini Kenya wanapendekezwa kuzingatia kwa uangalifu uteuzi na upangaji wa mandhari wakati wa utayarishaji wa kazi zao. Kwa kuwa mandhari yanaweza kubeba maana za kijamii, kiuchumi na kimaadili, uteuzi wake unapaswa kuhusishwa na maudhui na mwelekeo wa simulizi.

Wahakiki na watafiti wa fasihi na filamu za Kiswahili wanapendekezwa kutumia mkabala wa kisemiotiki katika kuchanganua kazi nyingine za kifilamu, hususan tamthilia za televisheni na filamu za mfululizo ambazo bado hazijapewa uzito wa kutosha kitaaluma. Tafiti zijazo zinapaswa pia kuchunguza kwa pamoja mandhari, mwanga, sauti, muziki, mavazi na upigaji picha ili kubaini namna vipengele hivi vinavyoshirikiana katika ujenzi wa maana.

MAREJELEO

- Balázs, B. (1952). *Theory of the film: Character and growth of a new art*. Dover Publications.
- Barlet, O. (2000). *African cinemas: Decolonizing the gaze* (C. Turner, Trans.). Zed Books.
- Barthes, R. (1972). *Mythologies* (A. Lavers, Trans.). Hill and Wang. (Original work published 1957)
- Barthes, R. (1977). *Elements of semiology* (A. Lavers & C. Smith, Trans.). Hill and Wang. (Original work published 1964)
- Bature-Uzor, N. A. (2018). Mise-en-scène and authenticity in Kunle Afolayan's *October 1*. *AFRREV IJAH: An International Journal of Arts and Humanities*, 7(3), 41–54. <https://doi.org/10.4314/ijah.v7i3.5>
- Bordwell, D., & Thompson, K. (2013). *Film history: An introduction* (3rd ed.). McGraw-Hill.
- Bordwell, D., & Thompson, K. (2017). *Film art: An introduction* (11th ed.). McGraw-Hill Education.
- Cook, D. A. (2016). *A history of narrative film* (4th ed.). W. W. Norton & Company.
- Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (4th ed.). SAGE Publications.
- Diawara, M. (1992). *African cinema: Politics and culture*. Indiana University Press.
- Gitonga, D. T. (Director). (2012). *Nairobi half life* [Film]. One Fine Day Films.
- Haynes, J. (2000). *Nigerian video films*. Ohio University Press.
- Kahiu, W. (Director). (2018). *Rafiki* [Film]. Big World Cinema.
- Karata, R., Muusya, J., & Mavisi, R. (2021). Vipengele vya ontolojia katika tamthiliya za Kiswahili: *Mashetani* (1971) na *Kivuli Kinaishi* (1990). *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 3(1), 293–306. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.268>
- Kariuki, J. (2018). Film as cultural economy in Kenya: Tourism, identity and employment. *Journal of African Cultural Studies*.
- Kariuki, J., & Kamwara, K. (2025). Uhakiki wa mandhari katika riwaya teule za Kiswahili: *Tumaini* na *Kala Tufaha*. *East African Journal of Swahili Studies*, 8(3), 1–14. <https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3940>
- Karthick, S. M. (2023). A semiotic analysis of *Avatar* movie. *Journal of Advanced Research in Journalism and Mass Communication*, 10(3&4), 8–15. <https://doi.org/10.24321/2395.3810.202309>
- Kung'u, S., & Gathigi, G. (2023, Aprili 7). Gynocentric lenses: Deconstructing gender-based violence from Kenyan soap operas. *Kujenga Amani, Social Science Research Council*. <https://kujenga-amani.ssrc.org/2023/04/07/gynocentric-lenses-deconstructing-gender-based-violence-from-kenyan-soap-operas/>
- Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (1999). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches*. Acts Press.

- Ntongai, J. K., Mavisi, R., & Nkumbo, D. (2025). Uchanganuzi wa aina za mandhari kifinominolojia katika riwaya ya Nguu za Jadi. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 6(1), 78–93. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.631>
- Peirce, C. S. (1931–1958). *Collected papers of Charles Sanders Peirce* (C. Hartshorne, P. Weiss, & A. Burks, Eds.; Vols. 1–8). Harvard University Press.
- Pramaggiore, M., & Wallis, T. (2005). *Film: A critical introduction*. Laurence King Publishing.
- Sabol, J. (2018). Theatrical mise-en-scène in film form. *Slovak Theatre*, 66(3). <https://doi.org/10.2478/sd-2018-0017>
- Saussure, F. de. (2011). *Course in general linguistics* (W. Baskin, Trans.; P. Meisel & H. Saussy, Eds.). Columbia University Press. (Original work published 1916)
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Press and Publicity Centre.
- Wainaina, L. (Director). (2018). *Supa modo* [Film]. One Fine Day Films.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.